Kampeini husaidia kueneza ufahamu

MULIKA TB MALIZA TB

Mulika TB! Maliza TB! ni kampeini kabambe inaendeshwa kitaifa ili kuimarisha ufahamu kuhusu Kifua Kikuu na idadi ya watu waliopimwa hadi maradhi hayo yatakapokomeshwa. Ishara ya mienge ilitolewa kwa kaunti 10 zilizoathirika zaidi kote Kenya ili kuashirikia kujitolea kwa serikali na washikadau wake katika harakati za kukomesha Kifua Kikuu.

Jifunze zaidi
http://nltp.co.ke/the-mulika-tb-maliza-tb-concept
au Mulika Maliza kwenye mtandao wa Facebook.

KENYA IS GETTING #LOUDER THAN TB

PAZA SAUTI KULIKO KIFUA KIKUU ni kampeini ya kimataifa iliyoanzishwa na Muungano dhidi ya maradhi hayo, ukiwaleta pamoja washirika wa kibinafsi na wa umma kuhamasisha wananchi na kupaza sauti kuhusu maradhi haya yanayoua. Mashirika arubauni yanajumuika katika kampeini hii ya **#LouderThanTB**, ikiwa ni pamoja na UNITAID, UNICEF, WHO, Médecins sans Frontières, Save the Children, Stop TB Partnership, na mengine mengi. Huduma yake ni kuleta ufahamu kuhusu maradhi ya Kifua Kikuu katika watoto na kutafuta njia bora za kuwatibu watoto.

Jifunze mengi kuhusu 'Paaza Sauti Kuliko Kifua Kikuu kutoka kwa **TB.org**, au tafuta **#LouderThanTB** kwenye mtandao wa Facebook, Twitter, au Instagram.

MULIKA TB MALIZA TB USAID TB ARC TB ALLIANCE

REPUBLIC OF KENYA

MINISTRY OF HEALTH

Kukomesha Kifua Kikuu kunaanza na kusikia.

Ni wakati wa kutafuta na kuwatibu watoto wanaougua Kifua Kikuu.

USAID TB ARC TB ALLIANCE

Kusaidia kutibu Kifua Kikuu, mtoto mmoja kwa wakati

Kulingana na Shirika la Afya Ulimwenguni, karibu watoto milioni moja ulimwenguni huugua maradhi ya Kifua Kikuu kila mwaka. Watoto wapatao 210,000 hufariki kutokana na maradhi haya yanayoweza kutibiwa na kuzuiliwa; hii ikiwa ni sawa na watoto wawili kila baada ya dakika tano. Hapa Kenya, karibu watu 7,000 waliougua Kifua Kikuu mwaka wa 2015 ni watoto wachanga. Watoto wetu wachanga wamo hatarini.

Sasa kuna madawa ya watoto

- Dawa bora za kutibu Kifua Kikuu kwa viwango vinavyostahili
- Dawa hizi huyeyuka ndani ya maji baada ya sekunde chache
- Dawa hizo zina ladha ya matunda na kwa hivyo, ni rahisi kumpa mtoto

Dawa hizi zimeimarishwa kutokana na zile zilizoko, hivyo kuifanya rahisi kwa wahudumu wa afya na wale wa watoto kuwapa dawa hizo kwa urahisi.

"Kwa tiba hizi zinazostahili, tunaweza kupiga hatua ya haraka katika kuwapata na kuwatibu watoto wanaougua Kifua Kikuu ili tuweze kuwa na Kizazi ambacho hakina Kifua Kikuu."

—Dr Cleopa Mailu, Waziri wa Afya, Kenya

Habari njema: Tunaweza kutibu Kifua Kikuu

Kifua Kikuu ni maambukizi yanayodhuru mapafu na yanaweza kuenea katika sehemu nyingine za mwili. Baadhi ya watu wanaugua Kifua Kikuu huku kwa wengine wengi, viini vya ugonjwa huo vimejificha na huenda vikasababisha ugonjwa baadaye. Mara kwa mara, watoto wanaougua Kifua Kikuu hawashughulikiwi ipasavyo na hukaa bila kupimwa au kutibiwa.

- Ikiwa mtu yeyote anaugua Kifua Kikuu, watu wote walio karibu naye wapaswa kupimwa
- Juhudi zapaswa kufanywa kupata sampuli ya kufanyiwa uchunguzi kutoka kwa kila mtoto. Hata hivyo, uchunguzi mkali unaweza kufanyiwa watoto wengi huku kukiwa na umakinifu kutoa uhakika wa afya yao
- Kuwa wa kujali; kuwa mwangalifu: sisitiza kwamba mtu anayeugua Kifua Kikuu apeleke watoto wake wapimwe haraka iwezekanavyo
- Muwe na mazungumzo baina yenu – toa ushauri na mawazo, na himiza wahudumu wa afya kuuliza maswali kuhusu watoto ambao huenda walikaribiana na wanaougua maradhi ya Kifua Kikuu
- Maradhi ya Kifua Kikuu katika watoto yanaweza kuonyesha dalili sawa na magonjwa mengine yanayowapata watoto; unapaswa kuwa makini zaidi
- **Peleka watoto wapimwe. IWAPO TUTAWAPATA, TUNAWEZA KUWATIBU!**

Angalia dalili, na uulize maswali

Dalili ambazo wazazi na wahudumu wanahitaji kuangalia:

- Kikohozi cha muda wowote
- Watoto wanaohisi kuchoka na wanyonge
- Kupungua uzito
- Homa au kutokwa na jasho usiku

KUMBUKA:
Kikohozi cha muda ni ishara ya kimsingi, lakini mtu aliye na maradhi ya Kifua Kikuu huenda akajihisi mwenye afya au huenda akakohoa mara kwa mara.

Je wanaougua Kifua Kikuu wako na watoto nyumbani? Basi waambie walete watoto wao wanaporudi kwa matibabu. Kupimwa ndio mwanzo, na ni rahisi sana kwa vile vituo vya ukaguzi wa maradhi ya Kifua Kikuu vimo kote nchini Kenya.